

<b>AFRICAN UNION</b>  <b>الاتحاد الأفريقي</b>  <i>African Commission on Human &amp; Peoples' Rights</i>		<b>UNION AFRICAINE</b>  <b>UNIÃO AFRICANA</b>  <i>Commission Africaine des Droits de l'Homme et des Peuples</i>
<p>31 Bijilo Annex Layout, Kombo North District, Western Region, P. O. Box 673, Banjul, The Gambia  Tel: (220) 4410505 / 4410506; Cellphone: (220) 230 4361  E-mail: <a href="mailto:au-banjul@africa-union.org">au-banjul@africa-union.org</a>; Web: <a href="http://www.achpr.org">www.achpr.org</a></p>		

Kumbukumbu: ACHPR/STC/OS/75/.../23 (e)

Tarehe: 04 Aprili 2023

**Taasisi zote za Kitaifa za Haki za Binadamu (NHRIs) barani Afrika**

**MWALIKO WA MKUTANO WA WAZI KWENYE MKUTANO WA KAWAIDA WA 75 WA TUME YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU TAREHE 03 - 13 MEI NA 23 MEI 2023**

Ninayo heshima kuzitaarifu Taasisi za Kitaifa za Haki za Binadamu (NHRIs zote zilizopewa hadhi ya uangalizi na Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu kwamba Mkutano wa Kawaida wa 75 wa Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu (Tume) utafanyika Banjul, Jamhuri ya Gambia, kuanzia tarehe 03 hadi 23 Mei 2023, na kuwaalika katika **Mkutano wa Wazi** uliopangwa kufanyika kuanzia tarehe **03 – 13 Mei 2023**, na Sherehe za Kufunga tarehe **23 Mei 2023**.

Mkutano wa Kawaida wa 75 utafanyika katika mfumo mchanganyiko. Wawakilishi wa NHRIs ambao watataka kushiriki kwa njia ya mtandao wanaweza kufanya hivyo kwa kutumia kiungo cha tovuti kifuatacho: [https://zoom.us/webinar/register/WN\\_9HFjHBQvTBeva3bt0x1Mzw](https://zoom.us/webinar/register/WN_9HFjHBQvTBeva3bt0x1Mzw)

Tafadhali zingatia kuwa NHRIs zinatarajiwa kulipia gharama zinazohusiana na kushiriki kwa wawakilishi wao.

Fomu ya Awali ya Usajili inaweza kujazwa mtandaoni kwenye tovuti ya Tume ya Afrika [www.achpr.au.int](http://www.achpr.au.int) chini ya sehemu "News and Media - Upcoming Events – 75th Ordinary Session". Taarifa yenye miongozo zaidi kuhusu Mkutano, Taarifa za Uzoefu na rasimu ya Ajenda ya Mkutano wa Wazi vimepakwa katika sehemu hiyo.

Wawakilishi wa NHRIs wanaotaka kushiriki kwa kuwapo kwenye Mkutano wanashauriwa kupata chanjo, na kusafiri na kadi zao za chanjo. Wawakilishi wanaotoka katika nchi ambazo zinahitaji viza ili kuingia karika Jamhuri ya Gambia, wanashauriwa kupata viza kabla ya kusafiri. Kwa wale ambao hawana Balozi au uwakilishi wa kidiplomasia wa Gambia katika nchi zao husika wanazokaa, hatua zitachukuliwa kuwezesha utoaji wa viza wanapowasili Banjul, ili mradi wawe wamewasilisha fomu zao za Usajili na nakala za ukurasa wa pasipoti zao wenye data za kibiolojia kwa Sekretarieti ya Tume.

NHRIs zinazotaka kuzunguza katika kipengele chochote cha Ajenda wanatakiwa kujiandikisha kwa Sekretarieti ya Tume mapema, na **kutuma kwa Sekretarieti nakala za taarifa** wanazotaka kuzitoa. Hili ni sharti la awali la kupewa ruhusa ya kuzungumza wakati wa Mkutano na lazima lifuatwe. Tafadhali zingatia kwamba ni NHRIs zenye Hadhi ya Uangalizi tu zitakazoruhusiwa kuzungumza mbele ya Tume.

**Wenu Mwaminifu**

**Ms. Lindiwe Khumalo**

**Kaimu Katibu Mendaji wa Tume**

em/LK